GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXIII Nam. **....., 2016** **Bei Shs. 3,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 2 ya 2005, kuweka masharti bora zaidi kwa ajili ya ufanisi na usimamizi imara wa Mfuko na mambo yanayohusiana na hayo..... 00

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada uliyotajwa hapo chini umetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya 2016,

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi ulioanza tarehe 21 Septemba, 2016 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
29th Agosti, 2016

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA

wa

SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII NAMBA 2 YA 2005, KUWEKA MASHARTI BORA ZAIDI KWA AJILI YA UFANISI NA USIMAMIZI IMARA WA MFUKO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya 2016, na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais.

Kusomwa.

2. Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Namba 2 ya 2005 ambayo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria mama".

SEHEMU YA PILI
VIFUNGU VYA MAREKEBISHO

Marekebisho ya Kifungu cha 2.

3. Kifungucha 2 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo-

(a) Kwa kufuta tafsiri ya neno "mshahara" na kuweka badala yake tafsiri ya neno "mshahara" kama ifuatavyo-

"mshahara" maana yake ni fedha anayolipwa mfanyakazi kwa kutumikia mkataba wake wa ajira"

(b) Kuweka tafsiri mpya ya maneno katika mpangilio wa herufi kama ifuatavyo-

"Mafao ya uzeeni pungufu" maana yake ni malipo ya pencheni na kiinua mgongo anayolipwa mwanachama aliyetimiza umri wa kustaafu na kuchangia kwa muda wa miezi sitini au zaidi, lakini chini ya miezi mia moja na hamsini na sita;

"Wastani wa mshahara wa mwisho" maana yake ni wastani wa mshahara wa miezi sitini bora kati ya miezi mia moja na hamsini na sita ya mwisho ya muda wa uchangiaji;

"Muda wa uchangiaji" maana yake ni idadi ya miezi ambayo michango imelipwa katika Mfuko;

"Uwiano wa rasilimali" maana yake ni jumla ya rasilimali mwisho wa mwaka kwa kulinganisha na jumla ya matumizi ya Mfuko katika kipindi cha mwaka husika;

"Ukomo wa kipato" ni kiwango cha juu cha mshahara kitakachotumika kukokotoa pencheni ambacho hupatikana kwa kuzidisha wastani wa mshahara wa kima cha chini wa Serikali mara ishirini na tano.

4. Kifungu cha 12 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo- Marekebisho ya Kifungu cha 12.

(a) Kuweka nambari upya ya aya ya (f) kuwa aya ya (g) kwa mpangilio;

(b) Kuweka aya mpya ya (f) kama ifuatavyo-

(f) "kuazima fedha kwa njia ya mkopo, "overdraft" au njia nyinginezo kwa lengo la kugharimia miradi kwa dhamana na masharti yanayohusiana na kurejesha mkopo huo kama Bodi itakavyoona inafaa".

5. Kifungu cha 17 (3) cha Sheria mama kinafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo- Marekebisho ya Kifungu cha 17.

(a) Kufuta Kifungu kidogo cha (3) na kuweka badala yake Kifungu kipya kidogo cha (3) kama ifuatavyo-

(3) "Kila mchango wa mwanachama utawasilishwa kwa utaratibu uliowekwa ndani ya siku kumi na tano baada ya mwisho wa mwezi".

(b) Kuweka Kifungu kidogo kipya cha (4) (a) na (b) kama ifuatavyo-

(4)(a) "Mtu yeyote anayekwenda kinyume na masharti ya Kifungu kidogo cha (3) cha Kifungu hiki, ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopunguwa milioni tano fedha za kitanzania au kifungo cha mda wa mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja";

(b) "pamoja na adhabu itakayotolewa kwa mujibu wa Kifungu cha (3) (a) cha Kifungu hiki, mahakama baada ya kumtia mtuhumiwa hatiani itamuamuru mtuhumiwa huyo kulipa kiwango stahiki cha deni la mchango analodai na mfuko pamoja na riba iliyopatikana kutokana na deni la mchango huo.

6. Kifungu cha 23 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo- Marekebisho ya Kifungu cha 23.

kuengeza kifungu cha maneno "kufanya mazingira ya ukaribu wa biashara katika muda muafaka" baina ya maneno "kuambatanisha" na "au mauzo".

7. Kifungu cha 26 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo- Marekebisho ya Kifungu cha 26.

(a) Kwenye Kifungu kidogo cha (1)-

(i) kufuta Kifungu cha maneno "kujumuisha mafao na kiinua mgongo" yaliyojiotokeza baada ya maneno "umri wa uzeeni" katika aya ya (a) ya Kifungu kidogo cha (1) cha Kifungu hiki;

(ii) kufuta Kifungu cha maneno "kwa ajili ya wategemezi" kilichojitokeza baada ya neno "maslahi ya walio hai" katika aya ya (b) ya Kifungu kidogo cha (1) cha Kifungu hiki;

(iii) kufuta neno "matunzo" lililojitokeza baina ya neno "tiba" na "maslahi" katika aya ya (e) ya Kifungu kidogo cha (1) cha Kifungu hiki:

(b) Kufuta Kifungu kidogo cha (3) cha Kifungu cha 26 na kuweka badala yake Kifungu kipya cha (3) kama ifuatavyo-

(3) "Waziri anao uwezo wa kucheleweshe mafao ya aina yoyote kutokana na sababu ambazo atajiridhisha kwamba mfuko hauna uwezo wa kulipa mafao hayo kwa wakati huo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii".

Marekebisho ya Kifungu cha 29.

8. Kifungu cha 29 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo-

(a) kufuta aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na kuweka badala yake aya (a)(i) na (a)(ii) kama ifuatavyo-

(a)(i) mara tu anapostaafu baada ya kufikia umri wa kupokea pencheni;

(ii) bila kuathiri masharti ya aya (a)(i) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki mwanachama aliye kwenye utumishi wa nyongeza atastahiki kupata pencheni na kiinua mgongo cha Mfuko baada ya kukamilisha utumishi wake huo wa nyongeza;

(b) Kufuta kifungu kidogo cha (7) na kuweka badala yake Kifungu kipya kidogo cha (7) kama ifuatavyo-

(7) "Namna na kiwango cha kulipa mafao yote yaliyotajwa chini ya sheria hii yataamuliwa kwa kanuni zitazotungwa na Waziri kwa kushauriana na Bodi".

(c)(i) kufuta nambari "sitini" lililojitokeza baina ya neno "angalau" na "miezi" katika Kifungu kidogo cha (8) na kuweka badala yake neno" elfu moja mia tano sitini";

(ii) kufuta neno " mafao" lililojitokeza mwisho wa Kifungu kidogo cha (8) na kuweka badala yake neno " mafao".

Marekebisho ya Kifungu cha 31.

9. Kifungu cha 31 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo-

(a) Kufuta Kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake Kifungu kipya kidogo cha (2) kama ifuatavyo-

(2) "Mwanachama aliyetimiza umri wa kustaafu, kupata ulemavu au kufa kabla ya kufikisha kipindi cha miezi sitini cha michango yake kwa Mfuko atastahiki kulipwa marejesho

ambayo ni sawa na wastani wa michango ya miezi ishirini na nne bora kwa mafao ya muda mrefu mara idadi ya miezi aliyochangia katika Mfuko".

(b) kufuta Kifungu kidogo cha (3) na kuweka badala yake Kifungu kipya cha (3) kama ifuatavyo-

(3) "Mwanachama aliyetimiza umri wa kustaafu, kupata ulemavu au kufa kabla ya kufikisha kipindi cha miezi sitini cha michango yake kwa Mfuko atastahiki kulipwa marejesho ambayo ni sawa na jumla ya michango aliyochangia kwa mafao ya muda mrefu".

(c) kufuta Kifungu kidogo cha (4) na kuweka badala yake Kifungu kipya cha (4) kama ifuatavyo-

(4) "Mwanachama aliyefikia umri wa kustaafu kabla ya kutimiza kipindi cha miezi mia moja na ishirini lakini katimiza zaidi au sawa na kipindi cha miezi sitini atastahiki kulipwa mafao pungufu ya uzeeni kama ilivyoelezwa katika jadweli la kwanza chini ya sheria hii".

(d) kuweka Kifungu kipya cha (5) kama ifuatavyo-

(5) "Mafao au marejesho ya warithi yanalipwa kwa warithi au mwakilishi binafsi kisheria kulingana na kifungu cha saba cha jadweli la tatu chini ya sheria hii".

(e) kuweka Kifungu kipya cha (6) kama ifuatavyo-

(6) "Iwapo mwanachama amefanya kazi kwa kipindi fulani na kwa sababu yoyote akasimamishwa kazi, michango ya mwanachama huyo haistahiki kurejeshwa isipokua izuiliwe na Mfuko kusubiri ukokotoaji wa mafao kipindi cha kustaafu, atakapopata ulemavu au kufariki".

(f) kuweka Kifungu kipya cha (7) kama ifuatavyo-

(7) "Waziri anaweza kwa kushirikiana na Bodi kuandaa kanuni zitakazowaruhusu wanachama walioacha au kuachishwa kazi kupewa mafao maalum bila kuathiri uendelevu wa Mfuko".

10. Kifungu cha 32 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta Kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake Kifungu kipya cha (2) kama ifuatavyo- Marekebisho ya Kifungu cha 32.

(2) "Wakati wa maombi ya mafao ya Mfuko yaliyotajwa katika kifungu cha 29 cha sheria hii, Mkurugenzi Mwendeshaji baada ya kujiridhisha na ushahidi wa maombi hayo, ataidhinisha kiwango cha fedha ambacho mwanachama anastahiki kulipwa".

11. Kifungu cha 41 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo- Marekebisho ya Kifungu cha 41.

(a) kuweka upya nambari ya kifungu cha 41 kuwa kifungu kipya cha 41(1) kama ifuatavyo-

41.-(1) "Jumla ya fedha iliyomo katika akaunti ya mwanachama wa Mfuko zinapaswa, kulingana na sheria hii, kubaki kuwa mali ya Mfuko na hazitokuwa sehemu ya rasilimali ya mwanachama, kwa hiyo hazitotumika itakapotokea kufilisika au kulipa deni hadi alipwe mwanachama husika".

(b) kuongeza Kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo-

(2) "Waziri anaweza, kwa kushauriana na Bodi, kuandaa kanuni zitakazowaruhusu wanachama kutumia stahiki ya mafao yao kama dhamana ya mkopo".

(c) kuongeza Kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo-

(3) "Mkopo unaotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki hautozidi asilimia hamsini ya stahiki ya kiinua mgongo katika kipindi cha maombi".

Marekebisho ya Kifungu cha 42.

12. Kifungu cha 42 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo-

(a) kuongeza kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo-

(3) "Mtu yeyote ambaye atashindwa kutekeleza masharti yoyote ya Sheria hii ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya milioni tano fedha za kitanzania au kutumikia kifungo cha muda wa mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja".

(b) kuongeza Kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo-

(4) “Mahakama imtake mtu yeyote atakeyitiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya sheria hii, bila ya kuathiri shauri lolote linalohusiana na madai inaweza kumuamuru kulipa madeni yatokanayo na michango pamoja na riba au adhabu inayotokana na michango hiyo, iliyothibitishwa kudaiwa na Mfuko katika tarehe ya kutiwa hatiani, na kiwango cha deni hilo lililopatikana kama itavyotozwa faini na litalipwa Mfuko kwa ajili ya wanachama husika”

Marekebisho ya Kifungu cha 44.

13. Kifungu cha 44 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 44 na kuweka badala yake Kifungu kipya cha 44 kama ifuatavyo-

44. “Waziri, kwa kushauriana na Bodi, anaweza kutayarisha kanuni za kuanzisha Mfuko wa hiari kwa ajili ya wafanyakazi walio katika sekta isiyo rasmi, waliojiajiri wenyewe, waliomo katika sekta iliyo rasmi, wastaafu na wazanzibari wanaoishi nje ya Tanzania”.

JADWELI LA KWANZA

Utaratibu wa Ukokotoaji Mafao

[Chini ya kifungu cha 26 (1)]

---

14. Jadweli la kwanza katika Sheria mama linafutwa na kuwekwa badala yake Jadweli jipya la kwanza kama ifuatavyo- Marekebisho ya Jadweli la kwanza.

1.-(1) Pencheni na kiinua mgongo zitakokotolewa kama ifuatavyo- Ukokotoaji wa Pencheni na kiinua Mgongo.

(a) Kwa mwanachama anaestahiki mafao ya uzeeni-

(i) Pencheni ni sawa na asilimia thelathini na sita ya wastani wa mwisho wa mshahara. Kutakuwa na ongezeko la asilimia mbili ya wastani wa mwisho wa mshahara kwa kila ziada ya miezi kumi na mbili kutoka miezi mia moja hamsini na sita ya uchangiaji;

(ii) Kiinua mgongo ni sawa na sitini mara pencheni ya kila mwezi iliokokotolewa katika kijifungu (i) ya kifungu kidogo hiki;

(iii) Kima cha chini cha Pencheni ni sawa na 30% ya kima cha chini cha mshahara wa Serikali;

(iv) Ukomo wa mshahara unaweza kutumika katika ukokotoaji wa pencheni.

(b) Kwa mwanachama anaestahiki mafao pungufu ya uzeeni.

(i) Pencheni ni sawa na asilimia mbili na nusu ya wastani wa mwisho wa mshahara au mshahara unaokubalika kukokotolea pencheni kwa kila miezi kumi na mbili iliyokamilika;

(ii) Kiinua mgongo ni sawa na themanini mara pencheni ya kila mwezi iliokokotolewa katika para (i) ya kifungu kidogo hiki;

(iii) Ukomo wa mshahara unaweza kutumika katika ukokotoaji wa pencheni.

(c) Kwa mwanachama anaestahiki mafao ya ulemavu:

(i) Pencheni ni sawa na asilimia mbili na nusu ya wastani wa mwisho wa mshahara kwa kila miezi kumi na mbili iliyokamika;

(ii) Kiinua mgongo ni sawa na themanini mara pencheni ya kila mwezi iliokokotolewa katika kifungu (i) ya kifungu kidogo hiki;

(iii) Kima cha chini cha Pencheni ni sawa na 30% ya kima cha chini cha mshahara wa Serikali;

Ukomo wa mshahara unaweza kutumika katika ukokotoaji wa pencheni.

(d) Kwa mwanachama anaestahiki mafao ya urithi.

Kiinua mgongo ni sawa na asilimia ishirini ya wastani wa mshahara wa mwisho mara muda wa kuchangia.

Mgawanyo wa Mafao.

Fedha zinazochangiwa na mwanachama na mwajiri zitagawanywa kwa ajili ya-

(a) Mafao ya uzeeni, urithi na ulemavu 17.0%

(b) Mafao ya uzazi 1.0%

(c) Mafao ya matibabu 2.0%

JUMLA 20.0%.

Viwango vya Michango.

(a) Kila mwanachama atachangia Mfuko asilimia saba ya mshahara wake wa mwezi na muajiri anapaswa kukata mchango huo kutoka katika mshahara wa muajiriwa wake.

(b) Kila muajiri atapaswa kuchangia asilimia kumi na tatu itakayokokotolewa kutoka katika jumla ya mshahara wa mwezi anaolipwa mwajiriwa.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya marekebisho haya ya Mswada unaopendekezwa yamekusudiwa kuimarisha mfumo wa Sheria kwa kufanya mabadiliko ambayo yataondosha mapungufu yaliyojitokeza katika Sheria ya Mfuko wa hifadhi ya Jamii Namba 2 ya 2005. Marekebisho haya yamedhamiria kutoa huduma bora kwa wanachama na kushajihisha uchangiaji wa michango wa wanachama.

Marekebisho ya Mswada yamefanyika kutokana na mapitio yaliyofanywa na uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa kupitia uendeshaji wa Mfuko kwa lengo la kuimarisha na kuleta ufanisi wa uendeshaji wa mfuko.

Marekebisho haya yanayopendekezwa yamejumuisha ripoti ya tathimini iliyoangalia mfumo wa pencheni na viinua mgongo. Kimsingi ripoti hii ya tathmini ilipendekeza kuwa, kwa ajili ya kuondoa malalamiko na vikwazo katika uendeshaji wa mfuko, ni busara yakafanyika marekebisho ya Sheria ili kukidhi mahitaji ya wanachama na kuimarisha maendeleo ya uendeshaji wa mfuko.

Marekebisho ya Mswada yanayopendekezwa yamekuja kufungua fursa kwa baadhi ya wananchi ambao kwa kipindi kirefu Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ilikuwa ni vigumu kuwahudumia, hivyo basi, kwa marekebisho haya wanachama wa sekta zisizo rasmi, wanachama waliojiajiri wenyewe, Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi

pamoja na makundi maalumu watapata fursa ya kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Pia, marekebisho haya ya Mswada unaopendekezwa umempa uwezo Mhe. Waziri kuanzisha mfuko mbadala wa uchangiaji ambao mfuko huu utakuwa ni wa hiyari na hatouanzisha mpaka baada ya kushauriana na Bodi; kimsingi mfuko huu una lengo la kupanua wigo wa hifadhi ya jamii kwa wananchi mbalimbali.

Vilevile, marekebisho haya ya Mswada unaopendekezwa yamejikita katika kuangalia upya utaratibu mzuri wa ukokotoaji wa pencheni, mafao, na viinua mgongo kwa wanachama wa mfuko. Aidha lengo la utaratibu huu mpya ni kuhakikisha usalama wa michango, uimarishwaji wa mfuko, uhamasishwaji wa utoaji wa michango pamoja na utolewaji wa mafao stahiki kwa wanachama na wanufaika wao.

Marekebisho haya yamefanywa katika kifungu cha 1, 2, 12,17, 23,26, 29, 31, 32, 41, 42, 44 na Jadweli la kwanza la Sheria hii.

ZANZIBAR **(DR. KHALID SALUM MOHAMED)**
29 August, 2016 ***WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO***
ZANZIBAR